# HABARI

Toleo Na. 25 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Aprili 2024

# na MATUKIO

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

## TFRA, WAZALISHAJI WA MBOLEA NCHINI WAWEKA MIKAKATI



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent akiwa katika picha na wazalishaji wa ndani wa mbolea mara baada ya kumaliza kikao kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 20 Machi, 2024. Kushoto waliokaa ni Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Mamlaka, Happines Mbelle na kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji wa ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja wa Mamlaka Louis Kasera.


NDANI>>

TFRA yawajengea uwezo watumishi Matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii 4

TFRA yaendelea kuvutia uwekezaji tasnia ya mbolea 6



WATUMISHI TFRA wapewa elimu ya mipango, usimamizi wa fedha na uwekezaji 8

# TFRA, WAZALISHAJI WA MBOLEA NCHINI WAWEKA MIKAKATI

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imekutana na kufanya mazungumzo na wazalishaji wa mbolea nchini ambapo wamejadili mustakabali wa tasnia ya mbolea wenye lengo la kupunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje yan chi ifikapo mwaka 2030.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent alieleza kuwa, kupungua kwa utegemezi huo kutapunguza matumizi makubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza shehena za mbolea na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye Uchumi wa Taifa na kufikia lengo la kuchangia asilimia 10 ifikapo 2030.

Laurent alieleza hayo wakati wa kikao baina ya TFRA na wazalishaji wa ndani wa mbolea kilichofanyika tarehe 20 Machi, 2024 katika ukumbi wa Mamlaka Jijini Dar Es Salaam.

Akizungumza mara baada ya kikao hicho Mkurugenzi Laurent alisema, maono ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ifikapo 2030 ni kuhakikisha nchi inajitegemea kwa asilimia 100 katika kupata pembejeo ya mbolea zinazozalishwa na viwanda vya ndani.

Alieleza kuwa ili kufikia azima hiyo, Mamlaka imekutana na wazalishaji hao ili kujadilia maeneo yenye changamoto yaweze kufanyiwa kazi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa hizo zitakazopelekea nchi kujitosheleza.

Laurent alibainisha kuwa, Ili kufikia ajenda 10/30: Kilimo ni Biashara, juhudi zinafanyika ili kuongeza kiasi cha mbolea inayotumika kwenye hekta 1 kutoka kg. 19 mpaka kufikia wastani wa kilo 50 kwa hekta moja.

Alisema wastani wa mahitaji ya mbolea kwa mwaka kwa sasa ni takribani tani 848,000 kwa mbolea zote na kueleza kuwa matarajio ya Mamlaka ni kuongeza matumizi ya mbolea ifikapo 2030 kutakakotokana na juhudi za Mamlaka katika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima elimu ya kanuni bora za kilimo kama zinavyoelekezwa na Maafisa Ugani wetu katika maeneo yao, wakulima kuhamasishwa



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (kulia) akifuatilia mjadala baina ya Mamlaka na wazalishaji wa ndani wa mbolea katika kikao kilichofanyika tarehe 20 Machi, 2024 Jijini Dar es Salaam.

kutumia mbolea zinazozalishwa nchini pamoja na bei ya bidhaa hiyo kuwa himilivu.

Kwa upande wake, Tosky Hans Mkurugenzi Mtendaji wa Minjingu Mining and fertilizer Ltd, aliipongeza Mamlaka kwa kuitisha kikao kilichoangazia namna tasnia ya mbolea nchini inavyoweza kuongeza uzalishaji na utoshelevu kulingana na mahitaji ya nchi.

Alisema huu ni mwanzo mzuri na kuishauri TFRA kuzingiza na kufanyia kazi yote waliyokubaliana ili yasaidie katika kufikia azma ya utoshelevu kwa mahitaji ya mbolea nchini na nchi jirani.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Hapco Tanzania Limited, Conrad Massawe alisema, TFRA imekuwa ikishirikiana na wadau kwa muda mrefu na kuhakikisha mkulima anapata mbolea bora na kwa bei himilivu na kueleza kikao kilichofanyika kimekuwa na manufaa makubwa na kuomba moto ulioanzishwa na Mamlaka uendelee.

Wakati huohuo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea Itracom, Nduwimana Nazaire alimpongeza Mkurugenzi Laurent kwa juhudi anazozifanya katika kutatua changamoto za wazalishaji wa mbolea nchini na kueleza kikao hicho ni mwendelezo wa yaliyojadiliwa wakati wa ziara ya kiongozi huyo kwenye viwanda vya mbolea nchini na Itracom ikiwepo.

Alisema mpaka sasa kiwanda cha Itracom kina uwezo wa kuzalisha tani laki 8 na wanatarajia ifikapo mwezi Juni, 2024 watakuwa wamekamilisha ujenzi utakaopelekea kuzalisha kiasi cha tani milioni 1 kwa mwaka na kubainisha wako katika hatua za mwisho za ujenzi wa kiwanda hicho.

Akitaja maazimio ya kikao hicho, William Ngereja Mjumbe wa Bodi ya Itracom alisema ni pamoja na TFRA kwa kushirikiana na wazalishaji wa ndani wa mbolea kuja na sera, kanuni na sheria zitakazosaidia kulinda wazalishaji wa ndani wa mbolea, namna bora ya kufikisha mbolea kwa wakulima, namna bora ya kuboresha unufaikaji wa ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali, namna bora ya kuagiza mbolea zinazotoka nje kama malighafi.

# TFRA, WAZALISHAJI WA MBOLEA NCHINI WAWEKA MIKAKATI



Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa Mamlaka ya Udibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Esther Kapakala akiwasilisha mada juu ya Sheria iliyoanzisha Mamlaka na Majukumu yake kwa wazalishaji wa ndani wa mbolea wakati wa kikao baina yao na Mamlaka kilichofanyika tarehe 20 Machi, 2024 Jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti Happiness Mbele akizungumza wakati wa kikao baina ya mamlaka na wazalishaji wa ndani wa mbolea mara baada ya kumaliza kikao kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 20 Machi, 2024.





# TFRA yawajengea uwezo watumishi Matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii

Imeelezwa kuwa, kuwa matumizi ya mitandao ya kijamii kwa karne hii hayaepukiki na kueleza kuna taarifa unazoweza kuziweka kwenye mitandao lakini pia zipo zile zisizotakiwa kuwasilishwa kwa njia hiyo.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent,alipokuwa akifungua mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii yaliyokuwa yakitolewa kwa watumishi wa Mamlaka tarehe 20 Machi, 2024.

Alieleza kuwa, Mamlaka imeona ni vyema kuwapitisha kwenye mafunzo hayo watumishi wake ili kuwajengea uwezo wa namna wanavyopaswa kutumia mitandao hiyo bila kuwaathiri wao binafsi pamoja na taasisi wanayoitumikia.

Aidha, aliwataka watumishi kutambua umuhimu, mahitaji, kanuni na taratibu zinazotawala kwenye mitandao ya kijamii na kuona njia sahihi za kuzitumia katika kuwasiliana kwetu.

Mwisho aliwataka watumishi kuwa makini katika kulinda akaunti za taasisi na zao binafsi ili zisidukuliwe na kutumiwa na watu wenye nia ovu na kusababisha hatari.

Akitoa mafunzo hayo, mwezeshaji Silyvester Domasa, Meneja wa Huduma za Habari za Kidijitali kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), aliwataka watumishi kuzijua vilivyo akaunti za taasisi ili kuwa na uelewa wa chochote kinachojadiliwa kwenye kurasa zao.

Aidha, aliwapitisha katika kufahamu, miongozo mbalimbali inayosimamia mitandao ya kijamii



Mkurugenzi Mtendaji, **Joel Laurent** akizungumza na watumishi kuhusu Matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki ya 2010, Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2025, Mwongozo wa matumizi ya mitandao ya kijamii Serikalini, Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma No.3 wa 2013, Waraka unaotoa mwongozo wa Serikali katika matumizi mbalimbali ya TEHNOHAMA na vifaa vinavyohusiana na teknolojia hiyo katika ofisi za Serikali.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kupitia Kurugenzi ya Huduma za Mamlaka na Kitengo cha Uhusiano, Mawasiliano na Elimu viliratibu mafunzo hayo ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Bodi inayosimamia Mamlaka hiyo.



Watumishi wa Mamlaka makao Makuu Dar es Salaam wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mtandao.

# TFRA yawajengea uwezo watumishi Matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii













Watumishi wa Mamlaka makao Makuu Dar es Salaam wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mtandao.

# TFRA yaendelea kuvutia uwekezaji tasnia ya mbolea



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent akifuatilia wasilisho kutoka kwa Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa TFRA, Esther Kapakala, wawekezaji kutoka nchini Uturuki walioonesha nia kuwekeza kwenye tasnia ya mbolea nchini tarehe 21 Machi, 2021.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent amekutana na kufanya mazungumzo na wawekezaji kutoka nchini Uturuki walioonesha nia kuwekeza kwenye tasnia ya mbolea nchini.

Akizungumza katika kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Mamlaka tarehe 21 Machi, 2024, Mkurugenzi Laurent alieleza kuwa, asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini inaingizwa kutoka nje ya nchi na asilimia 10 pekee inazalishwa nchini.

Alisema nia yao ya kutaka kuwekeza katika viwanda vya mbolea kutapunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi na hivyo kurahisisha zoezi la kuwahudumia wakulima kwa kuwapatia mbolea bora kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Akiwasilisha taarifa ya Mamlaka na kubaiisha fursa zilizopo kwenye uwekezaji katika tasnia ya mbolea, Esther Kapakala, Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi aliwahakikishia wawekezaji kuwa Tanzania ni sehemu sahihi kwa wao kuwekeza kutokana na kwanza kabisa utashi wa kisiasa unaoonesha nia ya viongozi kueka nguvu ya kukuza Sekta ya Kilimo.

Aliyataja mambo mengine kuwa ni, uwepo wa soko la mbolea kutokana na asilimia kubwa ya watanzania kujikita kwenye shughuli za kilimo, uwepo wa miundombinu bora kwa ajili ya kusafirisha bidhaa ndani nan je ya nchi zinazopakana na Tanzania, uwepo wa malighafi za viwanda husika, umeme wa uhakika na mengine mengi.

Alibainisha maeneo wanayoweza kuwekeza kuwa ni pamoja na kwenye ujenzi wa viwanda, kuwekeza kwenye biashara ya mbolea, kusambaza mbolea, kuwekeza kwenye elimu na uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea Pamoja na kwenye ujenzi wa maghala.

Kwa upande wake, ALi Ugur Ates Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji cha Mediterania (MEDITERRANIAN EXPORTERS ASSOCIATION AND CEO OF ALTIN ATES GROUP- Mwekezaji) aliishukuru Mamlaka kwa mwongozo na taarifa nzuri walizozipata na kueleza kuwa atakwenda kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wawekezaji wengine wa nchini uturuki ili waweze kufika na kujionea fursa za uwekezaji kwenye tasnia ya mbolea nchini Tanzania.



Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa TFRA, Esther Kapakala, (aliyesimama) akieleza majukumu ya Mamlaka na fursa za uwekezaji kwenye tasnia ya mbolea kwa Mwekezaji aliyeonesha nia kuwekeza kwenye tasnia ya mbolea kutoka nchini Uturuki katika kikao kilichofanyika tarehe 21 Machi, 2021.

# TFRA yaendelea kuvutia uwekezaji tasnia ya mbolea












Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (katikati) akiwa katika picha na Mwekezaji kutoka nchini Uturuki, ALi Ugur Ates (wa tatu kutoka kulia) na ujumbe alioambatana nao Pamoja na watumishi wa Idara ya Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja mara baada ya kumaliza kikao kilicholenga kuwapa mwanga wa fursa za uwekezaji kwenye tasnia ya mbolea wawekezaji hao.

# WATUMISHI TFRA wapewa elimu ya mipango, usimamizi wa fedha na uwekezaji

Kama inavyofahamika kuwa, tarehe 8 Machi, 2024 kila mwaka ni maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Katika kuadhimisha siku hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) iliwajengea uwezo watumishi wake katika eneo la fedha ili kuwakumbusha kujiwekea akiba na kuwekeza kusikohitaji nguvu kubwa.

Mafunzo hayo ya siku moja yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ndogo ya Wizara Jijini Dar es Salaam zilipo ofisi za Mamlaka tarehe 5 Machi, 2024.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent aliwataka watumishi kutumia mafunzo hayo katika kuwajengea fikra chanya ya kuweza kufikia dhana ya usawa katika Nyanja zote kama inavyoshauriwa na viongozi wa kitaifa na kimataifa.

"Tuwe tunajiuliza endapo kuna mahala tunaona tumelala kidogo katika masuala ya kijinsia basi tuamke" Laurent alisema.

Alieleza kuwa, ili kuweza kuwekeza, mtu yeyote anahitaji kuwa na uelewa/eimu juu ya uwekezaji hususani unaohusisha manunuzi ya hisa, kuweka amana, hatifungani na uwekezaji mwingine wote ili uweze kunufaika.

Akitoa mafunzo hayo, Mwezeshaji CPA, Emmilian Busara alisema ajira ni nzuri lakini zina ukomo na kuwakumbusha umuhimu wa kuwekeza na kuweka akiba itakayowawezesha kuendesha maisha yao mara baada ya ajira kukoma au kukutana na jambo litakalowatoa kwenye ajira.

CPA Busara, aliwataka watumishi kuweka malengo ya juu katika mipango yao huku akifafanua kuwa mafanikio ya mtu yanatokana na kile anachokusudia kukipata moyoni mwake, pia aliwashauri kuwa na vyanzo tofauti vya mapato ili kimoja kikisumbua unakuwa na uhakika wa kuingiza kipato kupitia chanzo kingine na hivyo kupunguza msongo wa Mawazo.

"Huwezi kufanikiwa zaidi ya unavyowaza, jitahidi kuwaza mambo makubwa maana huwezi kufanikiwa zaidi ya unavyowaza" Busara alisisitiza.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Victoria Elangwa aliwataka watumishi kuyaingiza Yale waliyojifunza kwenye matendo na si kuyatia kapuni, alisema watumishi wamehamasika sana kwa elimu waliyoipata na kuwashauri vijana waliobahatika kujifunza elimu ya uwekezaji katika umri mdogo kutumia fursa hiyo itakayowapa uhuru wa kifedha katika Maisha yao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka, Joel Laurent (kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa(kulia) wakifuatilia mafunzo ya mipango, usimamizi wa fedha na uwekezaji yaliyokuwa yakitolewa na mwezeshaji CPA, Emmilian Busara katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 5 Machi, 2024 Jijini Dar es Salaam.

# WATUMISHI TFRA wapewa elimu ya mipango, usimamizi wa fedha na uwekezaji







Watumishi wa Mamlaka Makao Makuu wakifuatilia mada kutoka kwa mwezeshaji CPA, Emmilian Busara tarehe 5 Machi, 2024

# WATUMISHI TFRA wapewa elimu ya mipango, usimamizi wa fedha na uwekezaji









Watumishi wa Mamlaka Makao Makuu wakifuatilia mada kutoka kwa mwezeshaji CPA, Emmilian Busara tarehe 5 Machi, 2024

# Wadau wa mbolea Arusha wajengewa uwezo biashara ya mbolea

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Kanda ya Kaskazini imetoa mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wazalishaji, wauzaji wa mbolea na waingizaji wa mbolea wa mkoani Arusha ikiwa na lengo la kuwajengea uelewa juu ya majukumu yanayosimamiwa na Mamlaka na jinsi ya kuendesha biashara ya mbolea nchini.

Akizungumza mara baada ya mafunzo hayo, yaliyohudhuliwa Tarehe 21/03/2024 na watu 57 Kanda ya kaskazini na Tarehe 25/03/24 Walikuwa 81 jumla 138, Gothard Liampawe, Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Kanda ya Kaskazini alisema lengo la mafunzo hayo ni kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo Sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia tasnia ya mbolea nchini.

Hata hivyo alisema kwa mujibu wa Sheria ya mbolea namba 9 ya mwaka 2009 inaitaka Mamlaka kuhakikisha inatoa mafunzo kwa wadau wao.

"Tumejifunza mada mbalimbali katika mafunzo haya, kwanza tumejifunza na kupata uelewa kuhusu Sheria iliyoanzisha Mamlaka na majukumu yake pamoja na uelewa juu ya mbolea wadau kuelewa maana na matumizi ya mbolea".

Pamoja na kutoa mafunzo hayo katika Mkoa wa Arusha Kanda hiyo iliandaa mafunzo mengine yaliyofanyika tarehe 25 Machi, 2024 na tarehe 2 Aprili, 2024 walifanya mafunzo hayo katika Ukumbi wa Kristo Mfalme mjini Moshi Mkoa wa Kilimanjaro mafunzo hayo yaliendelea mkoani Tanga.

Aidha, kwa upande mwingine meneja huyo alisema wanatarajia kukutana na wadau zaidi ya 261 kwa Kanda nzima ya kaskazini ili kuhakikisha wanazidi kutoa Elimu kwa wadau hao.

Kwa upande wa washiriki wamesema mafunzo haya yatawajenga na kuwa mabalozi wazuri kwa wakulima.

Wamesema kuwa, mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza ufahamu zaidi juu ya Sheria, matumizi sahihi na uhifadhi wa mbolea.

"unaposambaza mbolea za ruzuku zinazotolewa na serikali ni lazima upitie mafunzo ya namna gani unapaswa kuhifadhi mbolea, lakini pia taratibu za kuzingatia katika kusambaza mbolea za ruzuku"

"Sasa mafunzo haya yatanijenga Mimi kama mmiliki wa agrovet na vijana wangu ambao nitakuwa nao pale ofisini waweze kuelewa na kutambua kwamba mbolea inahifadhiwa kwa namna gani lakini pia mbolea inatumikaje shambani"



## Wadau wa mbolea Arusha wajengewa uwezo biashara ya mbolea










# TFRA Kanda ya kati yaja na mashamba darasa kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea

Katika kuhakikisha Sekta ya Kilimo inatimiza azma yake ya Agenda 10/30: Kilimo ni biashara kufuatia tija ipatikanayo kutokana na shughuli za kilimo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imeendelea kubuni mbinu za kuhakikisha wakulima wanazingatia kanuni bora za kilimo.

Hayo yamebainika kufuatia uanzishwaji wa mashamba darasa wilayani Nzega Mtaa wa makalome kata ya ijanija uliofanywa na Ofisi ya Mamlaka Kanda ya Kati kwa kushirikiana na wadau wengine wa kilimo.

Akiwataja wadau hao, Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya kati, Allan Mariki amesema ni kampuni za mbolea za ETG na Minjingu pamoja na Wakala wa Mbegu ASA.

Uanzishwaji wa Mashamba hayo umefanyika tarehe 21 Machi, 2024 ambapo mazao ya mahindi na alzeti yatatumika kuhimiza juu ya matumizi sahihi ya mbolea pamoja na kuzingatia kanuni zote za kilimo ikiwemo kuandaa mashamba kwa wakati, kupanda kwa mbolea, kupalilia na kukuzia mazao yao kwa wakati.

Pamoja na uanzishwaji wa mashamba hayo, katika mtaa wa Ipilili wilayani Nzega limefunguliwa ghala lambolea za ruzuku ambapo kampuni ya ETG itafanya shughuli zake za kuwahudumia wakulima.

Agenda ya serikali ifikapo mwaka 2030 ni kuongeza mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye pato la taifa kwa asilimia 10.










# TFRA Kanda ya kati yaja na mashamba darasa kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea







# Wafanyabiashara 133 wapatiwa Elimu ya Mbolea Mikoa ya Geita na Mwanza



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Ziwa, Michael Sanga (mwenye tai) akiwa katika picha na washiriki wa mafunzo ya mbolea yaliyofanyika Jijini Mwanza tarehe 19 Machi, 2024

Wafanyabiashara wa mbolea wapatao 133 wa Mikoa ya Mwanza na Geita wamejengewa uwezo kuhusu taratibu za kisheria na biashara ya mbolea ili kuongeza wigo wa utoaji huduma bora kwa wakulima na kuongeza utii wa sheria ya Mbolea kwa wafanyabiashara wa Kanda ya Ziwa.

Mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 19 – 20 Machi, 2024 katika ukumbi wa NYANZA COOPERATIVE UNION (1984) LTD Jijini Mwanza na katika ukumbi wa GEDECO uliopo Geita Mjini mtawalia yaliwanufaisha wafanyabiashara 61 wa Mwanza na wafanyabiashara 72 wa Geita.

Mafunzo hayo ambayo yaliendeshwa na timu ya Ofisi ya Kanda ya Ziwa ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli ya utoaji elimu kwa umma inayofanywa na mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Akieleza umuhimu wa mafunzo hayo kwa wafanyabiashara wa mbolea, Meneja wa TFRA Kanda ya Ziwa, Michael Sanga alisema mafunzo hayo yanajenga uelewa kwa wafanyabiashara kwa kuwa wana nafasi kubwa ya kuwashauri wateja wao ambao ni wakulima na hivyo wanapaswa kuwa na taarifa sahihi.

Aliongeza kuwa, mafunzo hayo, yanasaidia kuongeza usambazaji wa mbolea kwa kuongeza wafanyabiashara wapya wa mbolea ambao watatoa huduma ya kuuza mbolea kwa wakulima kwenye maeneo tofauti tofauti nchini.

Pamoja na hayo, TFRA Kanda ya Ziwa itaaendelea kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali ya wadau wakiwemo wafanyabiashara wa mbolea ili waweze kuwa na taarifa sahihi na kutoa huduma bora kwa wakulima na kuongeza utii kwa Sheria ya Mbolea Na.9 ya mwaka 2009 na Kanuni za mwaka 2011 na marekebisho yake.

Alisema miongoni mwa mada zilizofundishwa ni pamoja na Sheria ya Mbolea, Virutubisho vya mimea na rutuba ya udongo, aina za mbolea, Matumizi sahihi ya mbolea na pH ya udongo, Mbolea na mazingira, Sifa za ghala, Kanuni na taratibu za utunzaji wa mbolea na visaidizi vya mbolea, Utekelezaji Mpango wa Ruzuku ya Mbolea na Usajili na kupata leseni kwa njia ya mtandao na Utunzaji wa kumbukumbu.



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Ziwa, Michael Sanga (wa nne kutoka kulia) akiwa katika picha na washiriki wa mafunzo ya mbolea yaliyofanyika mkoani Geita tarehe 20 Machi, 2024 huku washiriki wakiwa wameshikilia vyeti vyao.

# WATUMISHI TFRA WAWATEMBELEA YATIMA/ WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM



Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa akizungumza na wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule ya Sekondari Jangwani kuwatia moyo na kuwataka kukazana katika masomo ili kufikia ndoto zao

Watumishi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wamewatembelea wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule ya Sekondari ya Jangwani ikiwa ni sehemu ya maahdimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Akizungumza shuleni hapo, Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka wa TFRA, Victoria Elangwa aliwataka wanafunzi hao kujiamini na kutambua kuwa wamepata fursa ya kuamua kuwa vile wanavyotaka kwa maisha yao ya mbeleni.

Victoria aliyasema hayo tarehe 7 Machi, 2024 alipokuwa akizungumza na wanafunzi hao kwa niaba ya wanawake alioambatana nao kutoka TFRA kwa ajili ya kuwatia moyo wanafunzi hao wa kike ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofikia kilele tarehe 8 Machi, 2024.

Alisema fursa waliyoipata ya kusoma katika shule ya jangwani ina uwezo wa kuwapa kile wanachotamani kitimie katika maisha yao kwani kila binadamu anapokuja duniani anakuwa na kusudi analopaswa kulitimiza ikiwa ni nafasi za uongozi katika sekta mbalimbali nchini, biashara na nyingine nyingi kulingana na maono ya kila mmoja kwa upekee wake.

"Ninapenda kuwatia moyo na kuwapongeza kwa kuwa mpo sehemu sahihi kwa ajili ya kutengeneza kesho yenu kupitia elimu mnayoipata shuleni hapa, tumieni fursa hii vizuri" Elangwa alikazia.

Katika kuwahamasisha wanafunzi hao kujiamini, Bi. Victoria aliwaongoza kuimba mistari iliyosema; I know I can, be what I wanna be, If I work Hard at it. I'll be where I wanna be na kuelezwa kupendezwa na motto wa shule hiyo unaosema "Disability is not inability"

Akitoa neno la shukrani Makamu Mkuu wa Shule, Paulina Aweda alieleza, ujio wa TFRA unaanzisha ukurasa mpya wa mahusiano baina yao na TFRA.

Alisema, shule ya Jangwani inatoa elimu jumuishi na kueleza ni miongoni mwa shule kongwe na kubwa ikiwa na jumla ya wanafunzi 1360 wa kidato cha 1 hadi 6 huku idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwa ni wanafunzi 110.

Alisema shule yao inaandaa wanasayansi wa kesho, wachumi na kila aina ya mwanamke anayetegemewa kuja kujenga taifa la siku zijazo.

Kwa upande wake, Meneja wa Kitengo cha Uhusiano wa Mamlaka, Matilda Kasanga alisema wanawake wa TFRA wanajisikia faraja sana kwa kufika na kuwatembelea wanafunzi hao.

Bi. Kasanga aliongeza kuwa, TFRA kama taasisi ya Serikali ina wajibu wa kujenga mahusiano mazuri na taasisi zingine za serikali na binafsi na hivyo kurudisha fadhila kwa jamii inayowazunguka.

Wakati huo huo watumishi wa Mamlaka kutoka Kanda ya Kaskazini wakiongozwa na Meneja wa Kanda, Gothard Liampawe waliwatembelea Watoto yatima wa kituo cha Nkoaranga na kutoa zawadi kwa watoto hao.

Vile kwa Kanda ya Kati mtumishi pekee mwanamke Tumaini Haramba aliambatana na watumishi wanawake wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA) zilipo ofisi za Mamlaka kwenda kufanya matendo ya huruma kwa watoto yatima wa kituo cha Igambilo mjini Tabora.



Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa (wa 5 kutoka kushoto) akiwa katika picha na watumishi na waalimu wa shule ya Sekondari Jangwani walipokwenda kufanya matendo ya huruma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaosoma shuleni hapo tarehe 7 Machi, 2024 ikiwa ni namna ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyofikia kilele tarehe 8 Machi, 2024.

# WATUMISHI TFRA WAWATEMBELEA YATIMA/ WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM



Makamu Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Jangwani, Paulina Aweda akitoa neno la shukrani kwa watumishi wa TFRA mara baada ya kupokea misaada kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shuleni hapo tarehe 7 Machi, 2024.




Afisa Utawala wa Mamlaka, Ruth Magesa (wanne kutoka kulia) akikabidhi misaada kwa Makamu Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Jangwani, Paulina Aweda (Kushoto kwake)



Wanafunzi wenye mahitaji Maalum wa Shule ya Sekondari Jangwani wakifuatilia neno lililokuwa likitolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa (hayupo pichani) walipowatembelea wanafunzi hao ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha wiki la wanawake lililofikia kilele tarehe 8 Machi, 2024.

# Wadau wa mbolea 133 Morogoro wafikiwa na elimu ya mbolea

Jumla ya wafanyabiashara na wadau wa mbolea 133 mkoani Morogoro wamejengewa uwezo wa masuala mbalimbali yanayohusiana na mbolea na kutunukiwa cheti cha kuhitimu mafunzo hayo yatakayowawezesha kufanya biashara ya mbolea kwa mujibu wa sheria.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku 2 yakihusisha mada iliyohusu Sheria ya mbolea, matumizi sahihi ya mbolea, utunzaji wa mbolea, Mpango wa mbolea za Ruzuku n.k.

Aidha, washiriki wa mafunzo hayo walitoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Morogoro ikiwa ni eneo la Mlimba, Malinyi, Ulanga, Ruaha, na maeneo mengine.




Maafisa Udhibiti Ubora wa TFRA Reymond Konga (kushoto waliokaa) na Azizi Mtambo (kulia) na wawakilishi wa Mbolea za ruzuku kanda ya Mashariki wakiwa katika picha na washiriki wa mafunzo ya mbolea yaliyofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro baada ya kutunukiwa vyeti vyao.




Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA, Raymond Konga akitoa elimu ya mbolea wakati wa mafunzo yaliyofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro chini ya uratibu wa TFRA Kanda ya Mashariki.

# Wadau wa mbolea 133 Morogoro wafikiwa na elimu ya mbolea



Afisa Udhibiti Ubora Bw. Aziz Mtambo akiwasilisha somo la utunzaji wa mbolea kwa washiriki wa mafunzo ya mbolea yaliyofanyika tarehe 22 Machi, 2024 Mkoani Morogoro.



Mwakilishi wa Ruzuku Mkoa wa Morogoro Bw. Daudi Kabudi, akiwasilisha somo juu ya Utekelezaji wa Mpango wa Mbolea za Ruzuku kwa washiriki wa mafunzo ya mbolea yaliyofanyika mkoai Morogoro hivi karibuni.



# Wanawake TFRA wawafikia Walimu/ wanafunzi wa Shule ya Sekondari Temeke kwa elimu ya mbolea



Diwani wa Kata ya Sandal, Christopher Mwansasu akiwa katika picha na watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na walimu wa Shule ya Sekondari Temeke mara baada ya kuhitimisha ratiba ya kutoa elimu ya mbolea kwa walimu na wanafunzi. Hapo ni mbele ya bustani ya mbogamboga na matunda ya shule.

Walimu wa shule za Sekondari Vetenari, Temeke, Sandari na wanafunzi wa shule ya ya Temeke wamepewa elimu ya mbolea na kuombwa kuwa mabalozi wema kwenye jamii zao juu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Elimu hiyo imetolewa na wawakilishi wa watumishi wanawake wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ikiongozwa na Gema Nganyagwa Afisa Udhibiti Ubora ikiwa ni moja ya shughuli zinazotekelezwa kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 machi, 2024.

Akizungumza wakati wa tukio hilo Diwani wa Kata ya Sandali Mhe. Christopher Mwansasu ameeleza kuwa, Tfra ni taasisi ambayo inayotambua na kushirikiana na jamii inayoizunguka katika hali zote.

Ameeleza kuwa, wamekuwa wakishirikiana sana katika shughuli mbalimbali za maendeleo na ndio maana wameona ni vyema kufika na kutoa elimu ya mbolea kwa wanafunzi wa shule hii iliyopo katika jamii yake.

TFRA wanatambua kuwa elimu inaanzia chini na ndio maana wamechagua kundi hili ili kupanda mbegu inayowaandaa na kuwaonesha fursa zilizopo kwenye tasnia ya mbolea.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Temeke, Ingia Mtenga, ameishukuru TFRA kwa kuichagua shule anayoisimamia na kutoa elimu kwa wanafunzi hao.

Amesema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 2767 miongoni mwao wanafunzi 501 ni wa kidato cha 5 na 6 huku ikiwa na jumla ya walimu 60 na walimu 28 wakiwa ni wanawake.

Katika kuonesha uelewa walioupata kupitia elimu iliyotolewa wanafunzi waliulizwa maswali ikiwa ni pamoja na kutaka kujua tofauti kati ya mbolea za viwandani na samadi na kuhoji ni mbolea ipi inafaa zaidi.

Aidha, walitaka kujua namna Mamlaka inavyowafikia wakulima wa vijijini kwa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea, kujua namna Serikali ilivyojipanga kutatua changamoto za upatikanaji wa mbolea za ruzuku uliojitokeza msimu wa kilimo 2022/2023 na changamoto ya kutokupatikana kwa baadhi ya mbolea pindi zinapohitajiwa na wakulima kwa kutolea mfano wa mbolea za Amidas.

Pia, wanafunzi hao walipenda kujua namna Mamlaka inavyodhibiti mbolea zinazozalishwa nchini lakini pia zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na kupewa majibu Mujarabu kwa maswali yote yaliyoulizwa kutoka kwa wanawake hao.



Diwani wa Kata ya Sandal, Christopher Mwansasu (katikati), Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari Temeke Ingia Mtenga(kushoto) na Afisa Udhibiti Ubora wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Gema Nganyagwa (kulia) wakiwa katika picha mafunzo ya matumizi ya mbolea katika viwanja vya shule ya sekondari Temeke yakiendelea tarehe 5 Machi, 2024 wanawake wakirithisha ujuzi kwa waalimu na wanafunzi

# Wanawake TFRA wawafikia Walimu/ wanafunzi wa Shule ya Sekondari Temeke kwa elimu ya mbolea



Waalimu wa shule za sekondari Sandal na Vertenali wakifuatilia mada zilizokuwa zikitolewa na watumishi wa TFRA walipopewa mwaliko na uongozi wa shule ya Sekondari Temeke kuhusu nia ya Mamlaka kutoa elimu ya mbolea kwa wanafunzi wa shule yao ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya siku ya wanawake duniani.



Wanafunzi wa kidato cha tano na sitawa shule ya Sekondari Temeke wakiwa tayari kwa mafunzo ya mbolea kutoka kwa watumishi wanawake wa TFRA ikiwa ni katuka kuadhimisha siku ya wanawake duniani tarehe 8 Machi, 2024.



Wanafunzi wa kidato cha nne mpaka cha kwanza wa shule ya Sekondari Temeke wakiwa tayari kwa mafunzo ya mbolea kutoka kwa watumishi wanawake wa TFRA ikiwa ni katuka kuadhimisha siku ya wanawake duniani tarehe 8 Machi, 2024

# HABARI KATIKA PICHA







**www.tfra.go.tz**